THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# Monitoring Learner Achievement at Primary School Level in Kenya

KISWAHILI SEHEMU (B)

## Gredi ya 4

REPUBLIC OF KENYA
MINISTRY OF EDUCATION

© KNEC 2020

GEUZA UKURASA

**JINA** ______________________________________________

**NAMBARI YA USAJILI** ______________________________________

**MAAGIZO KWA MWANAFUNZI**

1. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.

   **Muda: Saa 1 dakika 20**

**<u>KWA MATUMIZI YA MTAHINI</u>**

**JEDWALI LA ALAMA**

| **SWALI** | 1(a) | 1(b) | 2(a) | 2(b) | 2(c) | 3(a) | 3(b) | 4(a) | 4(b) | 4(c) | 5(a) | 5(b) | 5(c) | 6(a) | 6(b) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **Alama** | | | | | | | | | | | | | | | |

| **SWALI** | 6(c) | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 10 | 37 |
| **Alama** | | | | | | | | | | | | | | |

**©KNEC 2020**

## SEHEMU YA A

## ZOEZI LA I: KUSOMA KWA UFAHAMU

**1.** *Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.*

Hapo zamani za kale ndege wote waliishi mwituni. Walipendana na kufanya kazi kwa ushirikiano. Kila ndege alikuwa na kazi yake. Tausi alikuwa fundi wa nguo. Chiriku alikuwa mtangazaji wa habari, naye Kuku alikuwa daktari. Mwewe alikuwa mfalme wao.

Chiriku alitangaza mwaliko wa sherehe ya mwezi mpya. Tausi aliwashonea ndege wote nguo za kupendeza. Ndege wote walikutana kwa mfalme. Walikula na kunywa. Watoto wao walicheza kwa furaha. Sherehe ilipokuwa ikiendelea, mtoto wa Tausi alimkanyaga mguu mtoto wa Mwewe. Ilikuwa bahati mbaya. Mtoto wa Tausi aliomba msamaha. Kuku alimtibu mtoto wa Mwewe.

(a) Chiriku alikuwa mtangazaji naye Kuku alikuwa

______________________________________________

(b) Hadithi hii imekufunza nini?

______________________________________________

**2.** *Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.*

Sungura alikwenda sokoni kununua karoti. Alipokuwa akirudi alikutana na Tumbili saba. Tumbili walimwomba Sungura karoti. “Nina karoti themanini na nane. Nitawapa karoti thelathini na nne mgawane. Nitabakia na karoti hamsini na nne,” Sungura aliwaambia tumbili.

Tumbili waligawana karoti walizopewa. Kila mmoja alipata karoti nne. Zilibakia karoti sita. Kila Tumbili alitaka kuchukua karoti zote sita. “Kama mmeshindwa kugawana karoti sita zilizobakia, nitazichukua,” Sungura alisema. Tumbili walimshukuru sungura kwa kuwapa karoti. Walimrudishia karoti sita zilizobakia. Tamaa ya Tumbili iliwafanya wakose karoti sita.

(a) Sungura alikwenda sokoni kununua nini?

______________________________________________

(b) Andika hamsini na nne kwa nambari.

______________________________________________

(c) Kwa nini Tumbili walishindwa kugawana koroti sita?

---

**3.** *Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.*

Mkala aliwaalika rafiki zake kwenye sherehe ya siku ya kuzaliwa kwake. Shangazi Eda alimsaidia kuandaa vyakula mbalimbali. Kulikuwa na mihogo, maharagwe, mboga na maji ya matunda. Watoto walikula chakula chote kwa furaha. Baada ya chakula walikula matunda.

Mkala alikata keki huku akisaidiwa na Rehema. Aliwagawia rafiki zake keki huku Kamau akiwapiga picha. “Keki yako ni tamu,” Rehema alisema “Hii ni keki ya viazi vitamu,” Mkala alimwambia Rehema. “Keki ya viazi vitamu?” Kamau aliuliza kwa mshangao. “Naam, kaka yangu anajua kupika keki ya viazi vitamu,” Mkala alimjibu Kamau.

“Basi nitamwambia dada yangu aje kufundishwa kupika keki kama hii,” Kamau alisema. Baada ya kula keki na kunywa maji ya machungwa, watoto walicheza ili kunyoosha viungo vya mwili.

(a) Tunga sentensi kwa kutumia neno **muhogo**.

---

(b) Vyakula vilivyotajwa katika kifungu vina faida gani mwilini?

---

**4.** *Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.*

*(Ni jioni, mama amefika nyumbani kutoka sokoni. Anamkuta Suna sebuleni)*

**Suna:** Shikamoo mama!

**Mama**: Marahaba Suna. Naona umebeba nguo nyingi hapo. Unazipeleka wapi?

**Suna**: Mama, umesahau kwamba kesho tunaenda kuzuru mbuga ya wanyama?

**Mama**: Sijasahau. Nimeuliza tu unakozipeleka nguo nyingi hivyo.

**Suna:** Nataka kuzipiga pasi kabla ya kwenda kulala. Mwalimu alisema tutaanza safari mapema. Sitaki kuachwa na basi.

**Mama:** Vyema. Ila naona umebeba mzigo mzima! Barua ya mwalimu ilisema safari yenu ni ya siku moja tu. Hili ni sanduku zima!

**Suna:** Mama nawe! Hizi sare mbili ndizo unazoita mzigo? Acha basi nikuhesabie. Hii hapa ni shati moja la kuvaa nikienda, na lingine la kuvaa nikirudi. Hizi hapa ni kaptura mbili. Hizi nazo ni soksi. Hata sweta nimebeba mbili tu. Mwalimu alisema kwamba huko mbugani huwa na baridi wakati mwingine. Sasa, umeona sijabeba sanduku zima?

**Mama:** Haya Suna. Naona unajitetea kweli kweli. Basi maliza kazi yako ulale mapema, usije ukachelewa kuamka kesho.

**Suna:** Ndiyo mama. Asante.

(a) Suna na wenzake walikuwa wanaenda wapi?

____________________________________________________

(b) Andika mavazi **mawili** yaliyotajwa katika kifungu.

____________________________________________________

(c) Andika maneno **mawili** yanayoonyesha kwamba Suna ni mwenye adabu.

____________________________________________________

**5.** *Soma hadithi hii kisha ujibu maswali*

" Hujambo mtoto mzuri?" Mama mmoja alinisalimu nikienda shuleni.
"Sijambo. Shikamoo mama."
"Marahaba mwanangu." Tafadhali nibebee mkoba wangu. Nimechoka sana." Mama huyo alisema.
"Samahani mama, siwezi. Mwalimu na walezi wangu waliniambia nisibebe vitu vya watu ambao siwajui."
"Si wewe unaitwa Baraka?" Mama huyo aliuliza.
Nilishangaa niliposikia mama huyo akilitaja jina langu. Baada ya kutembea naye kwa muda mfupi, askari walifika ghafla na kumshika mama huyo.
Lo! Kumbe alikuwa amebeba simu bandia. Lazima alikuwa amesoma jina langu ambalo lilikuwa limeandikwa nyuma ya sweta yangu.

(a) Baraka alikuwa anaenda wapi?

______________________________________________

(b) Mama huyo alitumia ujanja gani kujaribu kumshawishi Baraka ambebee mkoba?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

(c) Unafiri ni nini kingetokea kama Baraka angebeba mkoba?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

**6.** *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Familia ya Bwana na Bibi Alfa ilikuwa jirani yetu. Familia hiyo ilikuwa ya watu watano. Walikuwa baba, mama na watoto watatu. Kitinda mimba wao Rita alikuwa rafiki yangu. Siku moja walitualika kwa chakula cha jioni. Tulipofika kwao tulipata wameandaa vyakula mbalimbali. Kulikuwa pia na sharubati ya maembe na ya machungwa. Niliinua bilauri haraka ili nijitilie sharubati. Bilauri hiyo iliniponyoka. Kwa bahati nzuri, Rita aliishika kabla ifike sakafuni. Nilishukuru sana.

Dada yangu Sifa alinishauri nisiwe na haraka. Nilisikiliza na kufuata ushauri wake. Nilipakua na kula taratibu. Sote tulikula tukashiba. Tulishukuru kwa mwaliko huo.

(a) Neno **taratibu** limetumiwa kumaanisha nini?

________________________________________

(b) Ni nini kichoandaliwa katika familia ya Bwana na Bibi Alfa?

________________________________________

(c) Kungetokea nini kama bilauri ingeanguka?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

**SEHEMU YA B**

**ZOEZI LA II : SARUFI**

**7.** Andika umoja wa sentensi hii.
Matunda haya ni matamu.

______________________________________________

**8.** Panga maneno yafuatayo ili kuunda sentensi sahihi.
nafuu sukari kwa Juma bei alinunua

______________________________________________

**9.** Kanusha neno lililopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:
Kendi <u>anachora</u> mti sasa.

______________________________________________

**10.** Ambatanisha neno na kinyume.

| **Neno** | **Kinyume** |
|---|---|
| panda | anua |
| cheka | toka |
| anika | shuka |
| ingia | lia |

**11.** Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao.
Charo na Kibe walifua nguo.

______________________________________________

**12.** Chagua neno linalofaa katika mabano kujaza nafasi.

(a) Megi alivaa sare ________________ (lake, yake).
(b) Alitembea ______________ (haraka, polepole) ili afike shuleni mapema.

**13.** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kukubali.
Hatutapanda miche.

______________________________________________

**14.** Weka alama **?** na **.** mahali panapofaa katika kifungu kifuatacho:
Likizo iliyopita nilijifunza kupika Je, wewe ulijifunza kupika pia

______________________________________________

**15.** Kapu hili linastahili kuwa na maneno ya aina moja. Pigia mstari neno ambalo **halifai** kuwa katika kapu hili.




**16.** Chagua neno lifaalo kujaza nafasi.

Bena alipongezwa na mlezi wake ________________________ alipanga nguo zake. (kwa sababu, lakini)

**17.** Chagua jibu linalofaa kujaza nafasi.

__________________________ nilichana nywele zangu. (Wewe, Mimi, Yeye)

**SEHEMU YA C**

**ZOEZI LA III: KUANDIKA**

Andika insha kuhusu SHULE YETU katika nafasi uliyopewa.

**HUU NDIO UKARASA WA MWICHO ULIOPIGWA CHAPA.**